**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KAGERA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA SERIKALI YA NYABISHENGE

**April, 2024**

**NYABISHENGE-KYERWA DC**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MKOA WA KAGERA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

**ananiasclemence@gmail.com**
**Mkuu wa Shule 0621 007 763/0755 668 025**
**Makamu Mkuu wa Shule 0764 814 402/0769 304 684**
**Patron 0762 338 223**

**Shule ya Sekondari Nyabishenge,**

**S.L.P 544.**

**Tarehe 08.04.2024.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ......................................**
**..........................................................................................**
**S.L.P ...........................................................................**
**..........................................................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYABISHENGE HALMASHAURI YA KYERWA MKOA KAGERA MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2024** na atasoma tahasusi ya HKL/HGLi/HGFa Ni shule ya wavulana tu kwa kidato cha Tano.

Shule ya Sekondari Nyabishenge ipo umbali wa Kilometa 30 Magharibi mwa Mji wa Kyerwa.Usafiri wa basi kutoka mjini Bukoba –Karagwe-Kyerwa unapatikana katika kituo cha mabasi Bukoba/Omurushaka Nauli ni Shilingi 10,000.00/5,000.00 Panda pikipiki ufikapo Isingiro-Kyerwa Shilingi 1,500.00

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 08.07.2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 31.07.2024.Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31.07.2024

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii kwa wanafunzi wa kidato Tano ni Suruali 2 nyeusi ( zisiwe modal na ziwe na turn up)
ii. Mashati 2 meupe mikono mirefu.
iii. Sare ya Michezo ni truck suit moja rangi ya blue.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi pair 2 vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali. ( usiwe na chuma)
vii. Sweta moja rangi ya kijivu.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali 2 na T-shirt 2 rangi ya kijani jeshi.
ix. Tai moja yenye michirizi mikubwa nyeupe na nyeusi
x. Tisheti (T-shirt) moja ya shule ya kuvaa siku ya Ijumaa rangi ya light blue yenye kola shingoni.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 8 aina ya counter books 3 quires.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka. Leta ream moja kila muhula.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi ya HKL/HGLi/HGFa orodha imeambatanishwa.
iv. Godoro lenye vipimo vya 2.5X6
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya damu ya mzee, blanket 1, foronya ya godoro 1lenye cover ya rangi ya Pink, chandarua 1 rangi nyeupe ya duara.
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani ya chuma, bakuli, kijiko na kikombe chenye ujazo was nusu Lita.
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.
ix. Sabuni ya maji ya kusafisha vyooni yenye ujazo wa Lita 5 Kila muhula.
x. Toilet papers 10 Kila muhula.
xi. Kwanja 1, jembe 1, Mopper 1 kwa mwaka, mifagio 1 wa ndani aina ya soft bloom na 2 nje aina ya chelewa. Mfagio wa nje leta mmoja kila muhula na brush 1 ya kusafisha sink la choo.
X. Sanduku la mbao/chumba la kufunga na kofuli

xi) Aje na vifaa vya usafi binafsi Sabuni, mafuta ya kujipaka, mswaki, dawa ya meno, dawa ya viatu , brush na Kandambili.
xii) Tochi.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000.00 |
| 2 | Tahadhari | 5,000.00 |
| 3. | Nembo | 5,000.00 |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000.00 |
| | **Jumla** | **80,000.00** |

**N.B Malipo haya yalipwe akaunti ya shule namba 31901100050 jina la akaunti NYABISHENGE SECONDARY SCHOOL**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- **Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya kwa ajili ya matibabu ya afya yake. Shule haitoi matibabu yoyote kwa mwanafunzi. Huduma ya matibabu ni jukumu la mzazi.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**
**Jina la Mkuu wa Shule ANANIAS R. CLEMENCE**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0621007763 au 0755668025**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0764814402 au 0769304684**
- **Mwandamizi Taaluma 0754752634 au 0692622720**
- **Mwandamizi Malezi 0769020174**

## SHULE YA SEKONDARI NYABISHENGE
## FOMU YA KUKUBALI NA KUTII SHERIA ZA SHULE

ANWANI..........................................................................................

Mimi............................................................... (Jina la mwanafunzi) nimepokea barua ya kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Nyabishenge kuanzia tarehe 13/08/2023 hadi 31/08/2023. Nakubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu. Baada ya kusoma na kuelewa sheria za shule, naahidi kuwa nitatii sheria hizo kama zilivyoainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Nyabishenge Endapo nitashindwa kutii sheria hizo hatua inayostahili ichukuliwe dhidi yangu

Natoa ahadi hii mbele ya Mzazi /mlezi wangu ambaye ametia sahihi yake hapa chini.

Jina la mwanafunzi ......................................... sahihi..........................................

Mimi............................................................... (Jina la mzazi /mlezi) ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, nakubali mwanangu ajiunge kidato cha Tano katika shule ya Sekondari Nyabishenge na kutii sheria za shule na naahidi kushirikiana na shule ili kuhakikisha tunatoa malezi bora kulingana na sheria hizo na nyingine ambazo hazikutajwa pia.

Iwapo sitakuwepo mimi likitokea tatizo ninaweza kuwakilishwa na

1. .................................................. ambaye ni ...........................................
2. ..................................................... ambaye ni .................................................

(Eleza uhusiano wako na wawakilishi hao).........................................................

Sahihi .....................................................

Tarehe............................................................

**SHULE YA SEKONDARI NYABISHENGE**
**KIAMBATANISHO B**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI...................................................... (Kama ilivyo kwenye Selform)
2. Tarehe ya kuzaliwa..................................................
3. Mahali alipozaliwa: Wilaya..................Kijiji ................ kata .........................
4. Anwani ya nyumbani ni ..................................................
5. Dini yake ...............................................................

**WAZAZI**/MLEZI
Jina …..................................... Anwani ................................................
Anaishi /Amefariki (kata isiyohusika)..................................................
Ni raia wa nchi ipi? Itaje ................................................ (Tanzania/nchi nyingine)

**MAELEZO YA AFYA**
Eleza kama una tatizo lolote linalohitaji msaada au linaloweza kuathiri utendaji wako wa kazi za kila siku pamoja na maendeleo yako ya masomo. Maombi maalumu yadhibitishwe na daktari.
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
................................................................................................................

**SHULE YA SEKONDARI NYABISHENGE**
**KIAMBATANISHO C**
**HATI YA UTHIBITISHO WA TABIBU (anayetambuliwa na serikali)**

Nathibitisha kwamba nimemchunguza mwanafunzi
Jina: .......................................................
Kinyesi...................... Matokeo.......................................................

Mkojo.................... Matokeo.......................................................
Macho.................... Matokeo.............................................

Damu.................... Matokeo.............................................
Mapigo ya moyo.................... Matokeo.............................................
Urine Pregnancy Test (UPT).................... Matokeo.............................................
Matatizo mengine kama yapo....................

**MATIBABU** Yafuatayo yametolewa (kama ni ugonjwa wa kudumu eleza)
...........................................................................................................................
...........................................................................................................................
...........................................................................................................................
...................................................................
Jina la tabibu: .......................................................Sahihi: ....................................

Tarehe.............................................................

Muhuri.............................................................